**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**


**SHULE YA SEKONDARI NOONDOTO**
**S L P 8525– LONGIDO**
**20/12/2025**

***Kumb No: NSS/F.J.I/2026/VOL.01/01***

***MKUU WA SHULE: 0714148413.***
***OFISI YA MALEZI: 0653416364.***


***Mzazi/mlezi wa …………………………………………………***

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NOONDOTO, WILAYA YA LONGIDO MKOANI ARUSHA.**

**1:0 HONGERA**

Ninayo furaha kukuarifu kwamba, umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Noondoto kwa mwaka 2026. Shule ya sekondari Noondoto iko wilaya ya Longido na umbali wa kilomita 85 kutoka mji mkuu wa wilaya. . Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **13/01/2026**, hivyo unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 13/01/2026.

**2:0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1. SARE YA SHULE (MAVAZI)**

Uvaaji wa sare ya shule ni muhimu na ni lazima kwa kila mwanafunzi, kwa kuzingatia mishono stahiki ya kiuanafunzi yenye heshima. Kinyume na hapo shule haitokubaliana na mashono ya kihuni mfano; sketi/suruali fupi zinazobana, sketi/suruali kutokuwa na marinda yaliyoelekezwa, suruali zisizo na turn-up na zilizoshonwa kwa mtindo wa mnyonyo.vile vile rangi sahihi ya kitambaa cha unifomu rejea kitambaa kilichobandikwa kwenye fomu hii. Kwa maelekezo zaidi ya sare fuata utaratibu uliowekwa hapa chini.

**2.2 WAVULANA**

**Aje na sare ya shule kama ifuatavyo;**

i) Aje na suruali(Uniform) mbili rangi za rangi ya **KIJIVU ILIYOKOLEA(DARK GREY)** kwa ajili ya kuvaa darasani, na suruali moja ya rangi NYEUSI ya kuvaa baada ya kutoka darasani. Suruali zote ziwe na marinda mawili kila upande, ziwe na mkunjo (turn-up) na kila suruali iwe na INCHI 15 au zaidi kwenye turn up (Suruali za minyonyo au zinazobana haziruhusiwi).

ii) Aje na shati mbili nyeupe za mikono mifupi.

iii) Aje na sweta moja rangi ya **KIJIVU ILIYOKOLEA**.

iv) Aje na T- shirt moja ya rangi ya KIJIVU ILIYOKOLEA, yenye shingo ya duara ya dukani na isiwe na maandishi yoyote.

v) Aje na tai MBILI za rangi ya KIJIVU zenye michirizi myeupe.

vi) Aje na viatu vyeusi vya ngozi pair mbili, vyenye kisigino kifupi, vinavyofungwa kwa kamba na viwe vyepesi.

vii) Aje na soksi jozi (pair) mbili za rangi rangi ya kijivu.

viii) Aje na mkanda wa kufungia suruali wa ngozi wenye rangi nyeusi.

ix) Aje na nguo za ndani ambazo ni; singlendi(vesti) nyeupe mbili pamoja na chupi zisizopungua mbili.

x) Mashuka mawili, kwa wavulana yawe ya rangi ya bluu.

xi) Aje na nguo za michezo ambazo ni; **TRACK SUIT YA RANGI YA NYEUSI** yenye michirizi mnyeupe, aje na jezi NYEUSI(bukta na tisheti zisizokuwa na maandishi) pamoja na raba za rangi yoyote kwa ajili ya michezo.

xii) Kwa wavulana aje na vifaa vya usafi binafsi ambavyo ni MOPPER MOJA(squiza), SOFT BLOOM MOJA, SURURU MOJA ikiwa na mpini, MFAGIO MMOJA ambao ni (MFAGIO WA UKINDU) pamoja na PANGA.

## 2.3 WASICHANA

Aje na sare ya shule kama ifuatavyo;

**i)** Aje na sketi mbili za rangi ya **KIJIVU ILIYOKOLEA (uniform)** kwa ajili ya kuvaa darasani, na sketi moja ya rangi NYEUSI ya kuvaa baada ya masomo. Sketi zote zinatakiwa kuwa ndefu zinazovuka magoti **(toka kwenye goti ongeza cm 30 kwenda chini), mkanda (belt) wa sketi usizidi inchi TATU, kila sketi iwe na mshono wa RINDA BOX mbele na nyuma.**

ii) Aje na shati mbili nyeupe za mikono mifupi. Kwa waislamu ziwe nusu kanzu nyeupe za mikono mirefu, na ushungi mweupe usio na mapambo (urembo) wa aina yoyote na mwanandani mweupe (mtandio hautakiwi). Vile vile kwa waislam waje shamba dress ambayo ni nusu kanzu ya kijivu na hijabu ya kijivu.

iii) Aje na sweta rangi ya RANGI YA KIJIVU iliyokolea.

iv) Aje na Tisheti moja ya rangi ya KIJIVU iliyokolea yenye shingo ya duara isiyo na maandishi ya aina yoyote.

v) Aje na tai ya rangi ya KIJIVU yenye michirizi myeupe.

vi) Aje na soksi (stocking) rangi nyeupe ndefu pair mbili.

vii) Aje na viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba, vyenye kisigino kifupi na vyepesi.

viii) Aje na nguo za michezo ambazo ni TRACK SUIT RANGI NYEUSI yenye michirizi mnyeupe na ISIYOBANA MAUNGO YA MWILI, aje na jezi rangi ya nyeusi (bukta na tisheti) zisizo na maandishi, pamoja na raba za rangi yoyote kwa ajili ya michezo.

ix) Aje na nguo za ndani ambazo ni; chupi tano, taiti tatu, na vesti tatu.
x) Aje na taulo za kike (PEDI)
xi) Aje na kanga au kitenge doti moja ( masai shuka haziruhusiwi).
xii) Mashuka mawili, Kwa wasichana yawe ya rangi ya pinki.
xiii) Kwa wasichana aje na vifaa vya usafi binafsi ambavyo ni MOPPER MOJA(Squiza),MFAGIO MMOJA ambao ni (chelewa) HARD BLOOM, SURURU na mpini wake, pamoja na FYEKEO.

**2.4 WOTE.**

**Aje na vifaa vifuatavyo kwa ajili ya usafi na matumizi yake binafsi;**

i) Ndoo (lita kumi) ya kuogea, dumu la lita tano kwa ajili ya kutunza maji ya kunywa, sabuni minara mitatu, mafuta ya kujipaka ya mgando, taulo, dawa ya meno na mswaki, rangi ya viatu, brashi ya viatu na kitana kwa ajili ya nywele.
ii) Aje na vifaa vya chakula ambavyo ni sahani (kontena) kikombe (vyote rangi NYEKUNDU) pamoja na kijiko.
iii) Aje na vifaa vya darasani kama ifuatavyo; kalamu za wino wa bluu au nyeusi zisizopungua kumi, penseli, rula, mathematical set, madaftari ambayo ni counter book, 2-quire (kumi na mbili), madaftari ya kawaida-kumi (msomi), dictionary ndogo (**STUDENTS DICTIONARY OXFORD)**, File la kutunzia mitihani na four-figure moja.
iv) Godoro la **Comfy** au **Tanfoam** lenye vipimo 2.5 kwa inchi 4 kwa futi 6.

v) Sanduku la chuma/bati(tranka) likiwa na kufuli kwa ajili ya kutunzia vifaa na nguo zake
vi) Aje na blanket nyepesi (siyo masai shuka) kwa ajili baridi wakati wa usiku
vii) Aje na kitabu cha Imani yake yaani; biblia au qurani
viii) Aje na REAM PAPER (A4) mbili, moja ya mistari na ya pili isiyo na mistari kwa ajili ya mazoezi na majaribio binafsi.
ix) Aje na Hela ya kunyoa nywele shillingi elfu 10,000/=.(elfu kumi) kwa mwaka mzima.
x) Aje na tsh.5,000/=( shilingi elfu tano) kwa ajili ya kitambulisho.
xi) Aje tsh.5,000/= kwa ajili ya nembo kwenye shati la shule
xii) Aje na tsh. 15,000/= kwa ajili ya t-shirt zenye nembo ya shule zitakazotengenezwa kiwandani.
xiii) Aje na tochi kwa ajili ya matumizi yake binafsi wakati wa usiku.

**NB; NGUO ZOTE ZA MWANAFUNZI LAZIMA ZIWEKEWE ALAMA NA MZAZI HUSIKA.**

- **Mwanafunzi mwenye changamoto za kiafya anashauriwa kuja na vithibitisho kutoka kwa daktari.**
- **Vile vile matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi, kumsafirisha na kumtibu mwanao haswa pale huduma inayopatikana shuleni ama zahanati iliyopo karibu na shule haitakidhi mahitaji ya matibabu yake.**
- **SIKU YA KUWATEMBELEA WANAFUNZI (VISITING DAY) ITAKUWA NI KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI NA SI VINGINEVYO.**

### 3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

- ❖ Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi ambayo ndiyo yenye dhamana ya kusimamia elimu chini ya ofisi ya Rais – TAMISEMI .
- ❖ Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yamefafanuliwa kwa maandishi na mwanafunzi atapewa nakala yake maratu atakaporipoti shuleni.

### 3.1. NI MARUFUKU KWA MWANAFUNZI KUFIKA SHULENI NA VITU VIFUATAVYO:

- Mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani
- Vyakula vya aina yoyote mfano;mkate,blue band,soda, juice n.k.
- Vipodozi vya aina yoyote
- Redio, simu za mkononi,kamera n.k.

### 3.2 Pamoja na hayo yote tajwa hapo juu mwanafunzi anapashwa kuzingatia yafuatayo;

- Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzake na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- Kushiriki kwa umakini wajibu wa kujisomea wakati wa usiku(Night preparations)
- Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa na walezi, viongozi wa wanafunzi pamoja na uongozi wa shule kwa ujumla.
- Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- Kutunza usafi wa mwili wako na wa mazingira ya shule.
- Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa ndani na nje ya shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
- Kutunza mali za umma.

### 3.3 MAKOSA YANAYOWEZA KUMSABABISHA MWANAFUNZI KUSIMAMISHWA AU KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
1. 2. Uasherati (mahusiano ya kimapenzi), usagaji na ushoga
2. Ubakaji
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile, uvutaji bangi, sigara, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
4. Kupigana au kupiga.
5. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
6. Kudharau picha za viongozi wa kitaifa
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kudharau wimbo wa Taifa na wa shule
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata, kutoa au kuharibu mimba ndani au nje ya shule


11. Kugoma, kuchochea, kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule na mali zake au mali ya mwanafunzi mwenzako au ya jamii.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. Mwanafunzi kuwa na au kumiliki simu ya mkononi.

**4 .0 MAMBO MENGINE MUHIMU YA KUZINGATIA**

a) Fomu maalum ya uchunguzi wa afya ya mwanafunzi (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa afya katika vituo vya afya vya serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni ikiwa imejazwa kikamilifu.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo,fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri, kukubaliana na sheria, kanuni na taratibu za shule.
d) Ni lazima mwanafunzi afike na mzazi wake siku ya kuripoti

**Ni muhimu kusoma kwa umakini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza.**

**KARIBUNI SANA**
**Mwl. RENATUS M. MBANZIBWA**
**MKUU WA SHULE**




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**JINA NA ANWANI YA MZAZI………………………………**

**MKUU WA SHULE**
**NOONDOTO SEKONDARI**

**S L P 8525**
**LONGIDO –ARUSHA.**

**YAH; KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NOONDOTO**

Nachukua nafasi hii kulishukuru taifa langu kwa kunichagua mimi ……………………………………………………………………na kunipatia nafasi ya elimu ya sekondari. Hii ni bahati kubwa na ninahaidi kujifunza kadiri ya uwezo wangu wote, na sitapoteza muda wangu wa masomo darasani au wa kazi za mikono kwa kuwa mvivu na kupuuza shughuli hizo.

Pia ninahaidi kutopoteza rasilimali za wazazi wangu,au walezi wangu au wafadhili wangu kwa kutosoma ipasavyo kuwa mtaalam wa taifa langu katika siku zijazo.
Nimezisoma na kuzielewa sheria za shule, taratibu na masharti ya kujiunga na shule ya sekondari ya ketumbeine. Na ninakudhibitishia nimeafiki sheria na masharti hayo na kwamba,nitaziheshimu kwa kutozivunja sheria na taratibu za shule kwa makusudi.
Endapo nitakiuka taratibu zilizoainishwa, sheria za shule zichukue mkondo wake.
Wako mwanafunzi mtiifu.

Jina la mwanafunz………………......................sahihi……………….tarehe………..

MZAZI. Jina………………………………sahihi ………………………tarehe.........

**NB. Wasilisha fomu hii kwa mkuu wa shule ili iwekwe kwenye jalada la mwanafunzi.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**
**NOONDOTO SECONDARY SCHOOL**
**(To be completed by a medical officer in respect of all form one entrant)**

Students name……………………………………………
Age ………………………………………………………..
Sex ……………………………….
Blood count (red and white blood cells)………………………………….

Urine analysis…………………………………………………………..
Syphilis……………………………………………………………
Tuberculosis (TB) test …………………………………………………
Eye test……………………………………………………………
Ears …………………………………………………………………
Chest …………………………………………………………………………………
Abdomen ……………………………………………………………………………………
…
Spleen ……………………………………………………………………………………….
Pregnancy test (girls only)………………………………………………………………

Any additional information e.g. physical defects, infections, chronic or family disease e.t.c……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………….
I certify that the above named student is fit to pursue secondary education.
Name of a doctor………………………………………………………
Signature ………………………………………………………..
Designation …………………………………………………………
Station/health centre……………………………………………………
Date ………………………………………………………………